



## ReCONNECT

ReCONNECT ni huduma ya bure inayotolewa na ReturnToWorkSA. Inaweza kusaidia kukuunganisha na huduma za jamii wakati msaada wa kipato ukisimama.

Huduma ya ReCONNECT inapatikana hadi kwa miezi 12. Wakati huu, Mshauri wa ReCONNECT anaweza kukusaidia kupata msaada wa huduma kwenye:

- kifedha
- kinyumba
- kujitolea
- kutafuta kazi (e.g. kuandika resume, kuomba kazi na njia za kuomba kazi)
- jinsi ya kujiandaa na mahojiano ya kazi (k.m. ujuzi wa mahojiano, wawakilishi)
- mafunzo na kukua
- msaada wa familia
- msaada nyumbani
- usafairi.

Ili kuzungumza na mshauri wa ReCONNECT katika Kiswahili pigia Kituo cha Ukalimani na Utafsiri wa Lugha (Interpreting and Translating Centre) kwa 1800 280 203 na waulize kuwasiliana na ReturnToWorkSA kwa 13 18 55. Hii huduma ya ukalimani inapatikana bila gharama.